# OFISI YA RAIS- TAMISEMI

Shule ya Sekondari Wariku
S .L. P 43
BUNDA
Tarehe…………………………..
Simu na, 0767653044/0752797776.

MZAZI/MLEZI WA…………………………………………………………………

**YAH:MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa mwanao……………………………………………………………………………….. Amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katrika shule ya Sekondari WARIKU. Unatakiwa kumleta mwanao tarehe 11/01/2021 bila kuchelewa.

Napenda kukumbusha kwamba mwanao amechaguliwa kujaza nafasi ambayo Watanzania wengi wa aina yake wamekosa na wanailillia. Ni muhimu kwako kumkumbusha mwanao ajue umuhimu wa nafasi hii. Aidha, yampasa mtoto wako ajue shule ni mahali pa KUSOMA NA KUJIFUNZA na si mahali pa kustarehe na kufanya vihoja.

**MAHITAJI:**

Anahitajika aje na vitu vifuatavyo:-

**SARE ZA SHULE**

**A: WAVULANA**

i. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi yenye mfuko mmoja upande wa kushoto.
ii. Suruali mbili (2) dark bluu zenye marinda mawili upande wa kulia na kushoto, mifuko miwili moja kushoto moja kulia na mfuko mmoja nyuma upande wa kulia.
iii. Mkanda wa ngozi wenye rangi nyeusi na soksi nyeusi.
iv. Viatu vyeusi na vya ngozi jozi mbili vya kamba vyenye kufunika miguu, viwe na visigino vifupi na visipige kelele wakati wa kutembea.
v. Sweta lenye rangi ya dark bluu na huvaliwa wakati wa baridi tu.

**B: WASICHANA**

i. Sketi mbili za dark bluu zenye rinda boksi nyuma na mbele na marinda madogo mawili kulia na kushoto. Sketi hizo ziwe ndefu kufikia vifundo vya miguu na ziwe na mfuko mmoja upande wa kulia.
ii. Soksi ndefu za rangi nyeupe, zisiwe na urembo.
iii. Mashati mawili meupe mikono mifupi na mfuko mmoja upande wa kushoto
iv. Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vya kamba vyenye kufunika miguu viwe na visigino vifupi na visipige kelele wakati wa kutembea.
v. Sweta lenye rangi ya dark bluu na huvaliwa wakati wa baridi tu.
vi. Rangi ya hijabu ifanane na shati la shule.

**SARE ZA MICHEZO**

i. Track suti ya bluu yenye mistari miwili mieupe pembeni.
ii. Raba nyeupe
iii. Soksi za michezo rangi ya bluu

**MAHITAJI MENGINE**

i. Daftari 11(counter books kuanzia quire two), kalamu ya wino wa bluu au nyeusi na kalamu ya risasi(penseli), kamusi ya kiingereza (Dictionary-Oxford) na mkebe wa Hisabati(mathematical set)
ii. Mchango wa chakula, meza pamoja na viti vitajadiliwa na kikao cha wazazi baada ya shule kufunguliwa
iii. Mwanafunzi aje na mchango wa taaluma kwa ajili ya walimu wa muda(part time teachers(Tsh 10000/= kwa mwaka au Tsh 5000/= kwa muhula wa kwanza tu.
iv. Mwanafunzi aje na RIMU (Ream) moja ya karatasi aina ya DOUBLE A A4)

**MAELEZO/SHERIA AU NGUZO ADILI ZA SHULE YA SSEKONDARI WARIKU**

Shule ya Sekondari Wariku ni ya kutwa. Baadhi ya wanafunzi huja kusoma na kurudi nyumbani kwao. Wanafunzi wa mbali hupangishiwa vyumba na wazazi/walezi wao. Aidha shule ni ya mchanganyiko wavulana na wasichana. Shule ya sekondari Wariku ipo umbali wa kilometa 15 kaskazini mwa Mji wa Bunda njia iendayo Saragana hadi majita.

MAELEZO MAFUPI

Ndugu mzazi/mlezi, napenda kukumbusha tena mwano amechaguliwa kujaza nafasi ambayo Watazania wengi wa aina yake wanaililia sana. Mkumbushe mwanao aone umuhimu wa nafasi hii. Ni ukweli usiopingika kwamba malezi ya mwanafunzi **KITAALUMA, KIROHO na KIMWILI** yanategemea sana ushirikano kati ya walimu na wazazi/walezi. Hapa shuleni hakuna nafasi ya STAREHE na VIOJA-mahali pa kazi. Ukosefu wa mawasiliano baina ya pande mbili daima huzua/hutengeneza watendaji wasio na ELIMU wala UJUZI.

Uongozi wa hule umeona ni vizuri kuwashirikisha wazazi/walezi katika malezi ya watoto wao, hasa katika kuelewa **sheria, kanuni** pamoja na **taratibu** mbalimbali zinazotawala jumuiya ya shule ya sekondari Wariku.

Hivyo, nakuletea sheria au nguzo adili za shule, uzisome na kuzielewa, aidha mwanao ya mbidi kuzisoma na kukiri mbele yako kuwa yupo tayari kuzitekeleza . Mwisho baada ya kusoma mzazi unaombwa kuweka jina na sahihi yako, pamoja na mtoto wako naye aweke jina na sahihi yake na kipande hicho kirudi shuleni.

**SHERIA,NGUZO ADILI ZA SHULE YA SEKONDARI WARIKU**

**1. MASOMO**

(a) Mwanafunzi anatakiwa kusoma masomo yote aliyopangiwa na walimu

(b) Mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vipindi vyote nane(8) kwa siku sawa na vipindi 40 kwa wiki. Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya darasa bila ruhusa ya mwalimu isipokuwa wakati wa mapunziko mafupi tu. Kila baada ya masomo patakuwepo na parade saa 8:30 mchana kwa ajili ya matangazo na kuadhibu watoro na wachelewaji.

Mwanafunzi atakayekaidi na kuvunja sheria hii(a & b) hapo juu akaenda nje ya darasa bila ruhusa ataadhibiwa vikali.

(c) Lugha itumikayo ni kiingereza tu.

**2. MIPAKA**

Kwa mwanafunzi anapofika saa 12:45(saa kumi na mbili na dakika arobaini na tano asubuhi) haruhusiwi kwenda nje ya shule wakati wa vipindi bila ruhusa ya Mkuu wa shule/mwalimu wa zamu.

3. **HESHIMA**

a. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri. Anapopita mgeni bila ruhusa ya uongozi wa shule anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano ikumbukwe kuwa hairuhusiwi kuleta/kuongea na mgeni bila ruhusa ya ofisi.
b. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya, wakati wowote kati yao wenyewe, kwa walimu na kwa watu wengine.
c. Mwanafunzi awaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wake.
d. Mwanafunzi anatakiwa kushirikiana na kusaidiana katika kazi na wenzake.
e. Mwanafunzi anatakiwa kuthamini kazi ya aina yoyote.
f. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya yafuatayo:-
    - Kuvuta sigara
    - Kufuga kucha na kuwa na nywele zisizowekwa katika hali ya usafi. Wavulana wawe na nywele zenye urefu usiozidi sm 1 pia wavulana hawaruhusiwi kunyoa kipara. Endapo mwanafunzi atanyoa kipara ataadhibiwa. Wasichana hawaruhusiwi kusuka . Pia hawaruhusiwi kukali, kupaka wanja, kupaka midomo rangi na kusuka rasta.
    - Kufuga ndevu
    - Kuvaa mavazi yasio na heshima.
    - Kugombana

g. Mwanafunzi anatakiwa kuitikia mara moja na kukimbia aliko mkuu anayemwita.

h. Mwafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa (serikali), picha za viongozi wa serikali, nembo ya Taifa (coat of arms), wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.

i. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu ukumbi wa mikutano, ofisi za shule, mali binafsi na mali ya umma.

j. Mwanafunzi anatakiwa kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia mahali popote alipo.

**4. KUWAHI.**

a. Mwanafunzi anatakiwa athamini muda.
b. Mwanafunzi anatakiwa kuwa kwenye shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba kila siku. Uchelewaji haukubaliki.
c. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi asikiapo wito wa dharura.
d. Mwanafunzi anatakiwa kufika shuleni kwa tarehe iliyopangwa.

**5. SARE YA SHULE**

a. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa nguo rasmi za shule muda wote akiwa darasani na kwenye shughuli za kishule kama vile maandamano kwenye masomo ya ndani na nje ya shule. Akiwa amevaa nguo za shule (uniforms) haruhusiwi kujipamba na urembo wa aina yoyote ile kama vile hereni, mikufu, kofia, bangili, pete na rangi za kucha.
b. Ni marufuku kuvaa kanga, vitenge au sweta vazi lisilo la shule. Atakayekaidi sheria (a & b) hapo juu atapewa adhabu na walezi wake. Aidha mavazi hayo yatachukuliwa na kuhifadhiwa mpaka mwisho wa mwaka.
c. Wasichana watavaa sketi dark bluu.
d. Viatu vyeusi vyenye visigino vifupi kwa wavulana na wasichana (viatu vya ngozi). Wasichana watakuwa na soksi nyeupe (stocking) & wavulana pia.

## 6. MADARASA NA MAKTABA

- Madarasa na maktaba ni mahali pa masomo. Kwa hiyo ni marufuku kwa mwanafunzi kupiga kelele katika maeneo hayo.
- Ni marufuku kwa mwanafunzi kuzurura ovyo wakati wa masomo.
- Kuwahi darasani , utii kwa kengele na kuwahi unapotakiwa ni muhimu na ni lazima kwa mwanafunzi.

## 7. MAHUDHURIO

- Mwanafunzi anapaswa kufika shule siku ya kufungua shule.
- Mwanafunzi afikapo shuleni asubuhi atapaswa kuhudhuria "roll-call" zifuatazo:-
  a. Parade ya asubuhi saa 1:40 asubuhi kabla ya kuingia darasani.
  b. Mwisho wa masomo saa 7:50 mchana anatakiwa kuhudhuria parade ili kupokea maagizo ya siku inayofuata.
  c. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie **"parade ground"** kila siku za masomo **Asubuhi** na **Mchana**. Mwanafunzi asiyehudhuria sehemu hizo atahesabiwa kuwa ni mtoro na kuadhibiwa na uongozi wa shule.

## 8. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULENI

a. Wizi
b. Uasherati,ubakaji, na ushoga.
c. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
d. Uvutaji wa bangi, cocaine na mandrax.
e. Makosa ya jinai.
f. Kupigana na kupiga.
g. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
h. Kudharau bendera ya Taifa.
i. Kuoa au kuolewa.
j. Kupata mimba (wasichana) au kusababisha mimba ndani au nje ya shule.
k. Kutoa mimba.
l. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu.
m. Kukataa adhabu kwa makusudi.

Mwisho, mzazi/mlezi mawasiliano yako na uongozi wa shule ni muhimu katika kumlea mwanao kitaaluma,kimwili na kiroho. Hivyo, unaombwa uwe na mawasiliano na uongozi wa shule kila unapopata utata.

Napenda kukujulisha kuwa shule kwa muhula wa kwanza itafunguliwa tarehe………/………/……………..mwanao akichelewa kufika shuleni atapoteza nafasi hiyo. Tarehe ya mwisho ni…………/…………/…………….. baada ya hapo nafasi yako itachukuliwa na mwingine.

9. **MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUTEMBELEA SEHEMU ZIFUATAZO BILA KIBALI**

i. Ofisi ya shule.
ii. Maabara.
iii. Chumba cha walimu.
iv. Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

**USAFI**

Kila mwanafunzi anatakiwa kujali na kutunza usafi wa mazingira ya shule.

10. **BIASHARA NDANI YA SHULE.**

a. Ni marufuku kufanya biashara ndani ya shule (hairuhusiwi) hii humrudisha mwanafunzi nyuma kitaaluma.
b. Kuja na chakula chochote ili kuepukana na magonjwa ya mlipuko.

**SHERIA NA KANUNI NYINGINE**:-

Walimu wanaweza kwa idhini ya ushirikiano wa uongozi wa shule kuongeza sheria na nguzo adili za shule zingine ambazo kuwapo inapobidi. Nazo pia lazima mwanafunzi azitii na kuziheshimu endapo zitajitokeza.

**NB:** Mwanafunzi awapo shuleni anatakiwa kuzungumza lugha ya kiingereza tu na Kiswahili wakati wa kipindi cha Kiswahili tu darasani.

Nakutakia maandalizi mema, karibu **Wariku Sekondari,** shule nzuri na bora kitaaluma. Kumbuka, **Elimu ni Mali.**

…………………………………………………….

**MWIKWABE S. MSAMBA**

**MKUU WA SHULE**

**Tarehe**………/………../………………

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A**:

TO,The Medical Officer Date…………………………………………

……………………………………………………….. From…………………………………………

…..…………………………………………………….

…..………………………………………………………

Mr/Mrs/ Miss……………………………………………………………………………………………………………………..

(**Name in Full**)

Please examine the above as to his/her physical and mental fitness for a full time in studying as a secondary student. The examination should include the following:-

Categories (I)-(iii) each category or sub-category of which will surrender the applicant ineligible in case of defect. Pregnancy(category iv) will render a girl- candidate ineligible for students.

(1) (a) Eye - sight (b)Hearing (c) Limbs (d) Speech (e) Veneral Disease (f) Leprosy (g) Epilepsy

(2) Cirrhosis……………………………………………………………………………………………………………………………

(3) Other serious disease……………………………………………………………………………………………………………

(4) Pregnancy…………………………………………………………………………………………………………………………..

**PART B:**

**MEDICAL CERTIFICATE:**

**(To be completed by Government Medical Officer)**

I have examined the above named and consider that he/ she is physically FIT/UNFIT and mentally FIT/UNFIT for a full time studying course .

(i) (a) Eye sight……………………………………………………….. (b)Hearing………………………………………………………….

(c) Limbs……………………………………………………… (d)Speech …………………………………………………….

(e)Veneral diseases………………………………………… (f)Epilepsy………………………………………………………..

(ii) Neurosis……………………………………………………………………………………………………………………….

(iii) Other serious diseases………………………………………………………………………………………………………

(iv) Pregnancy……………………………………………………………………………………………………………………….

DATE……………………………………………………………………………. SIGNATURE………………………………………………….

STATION…………………………………………………………………. DESIGNATION……………………………………………………

**OFISI YA RAIS- TAMISEMI**

**IDARA YA ELIMU SEKONDARI**

**SHULE YA SEKONDARI WARIKU**

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI NA MKATABA WA KUTOSHIRIKI MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.**

Mimi………………………………………………………….. wa kidato cha…………………………… mwaka…………………..ninaahidi, katika maisha yangu ya uanafunzi katika shule ya sekondari Wariku, sitashiriki migomo ya aina yeyote ile na wala sitakataa

adhabu itakayotolewa dhidi yangu kutokana na makosa nitakayo tenda nikiwa mwanafunzi.

Pia ninaahidi kwamba sitashiriki au kusababisha fujo ya aina yoyote ile shuleni vilevile sitashiriki kutenda makosa ya jinai.

Sahihi ya mwanfunzi: ……………………………………………………………………………….. Tarehe……………………………………………….

Mimi………………………………………………………………………. Mzazi/mlezi wa mwanafunzi………………………………………………….

Wa kidato cha …………………………………… mwaka ……………………….. mwanangu hata shiriki migomo, fujo , na makosa ya jinai kama yeye mwenyewe alivyo ahidi.

Ikitokea amekiuka, hatua kali za kinidhamu zichukuliwe dhidi yake.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi………………………………………………… Tarehe…………………………………………………

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA**

**IDARA YA ELIMU SEKONDARI**

**SHULE YA SEKONDARI WARIKU**

**FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKUBALI MWANAE KUJINGA NA KIDATO CHA KWANZA 2020**

1. Mimi………………………………………………………. Baba/Mama/Mlezi wa……………………………………………… Ninayeishi Halmashauri ya Mji wa…………………………… Mtaa wa……………………………….…Kata ya……………………………… kubali mwanangu…………………………………………………… Ajiunge na shule ya sekondari Wariku.

2. Mimi…………………………………………………… Mzazi/Mlezi wa kijana huyu naahidi kushirikiana na walimu katika malezi ya mwanangu akiwa shuleni na hata akiwa nje ya shule.

3. Nakiri kwamba, kila mwisho wa muhula nitamtaka mwanangu anipe taarifa ya maendeleo yake kitaaluma na tabia.

**JINA LA MZAZI/ MLEZI**……………………………………………….. **SAHIHI YA MZAZI/MLEZI**…………………………………………

Mimi……………………………………………Mzazi/Mlezipamojanamwanangu……………………………………..(mwanafunzi), tumezisoma , tumezielewa na kukubali taratibu, sheria au nguzo adili za shule ya sekondari Wariku. Aidha mtoto yupo/hayupo tayari.

**JINA LA MZAZI/MLEZ**I…………………………………………………….. **SAHIHI YA MZAZI/MLEZI**……………………………………………

**JINA LA MWANAFUNZI**………………………………………………….. **SAHIHI YA MWANAFUNZ**I………………………………………

**TAREHE**…………………………………………………. **NAMBA YA SIMU** ………………………………………………………………..

KABLA YA KUJAZA FOMU HII NAOMBA MSHAURIANE KWA MAKINI WEWE MZAZI/MLEZI NA MWANAO ILI ISIJE IKAWALETEA MATATIZO ENDAPO HATA TII ADILI/ SHERIA ZA SHULE.

**NB: Fomu hii, mtoto afike nayo siku ya kufungua shule bila kukosa.**